HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA TAREHE 30/01/2020

Wajumbe waliohudhuria

1.	Mhe. Pascal M. Kihanga	__	Mstahiki Meya -Mwenyekiti
2.	Ndg. Sheilla E. Lukuba	__	Mkurugenzi wa Manispaa -Katibu
3.	Mhe. Isihaka Sengo Mtandikile	__	Naibu Meya - Mjumbe
4.	Mhe. Spear A. Komanya	__	Mjumbe
5.	Mhe. Zahara S. Kitima	__	Mjumbe
6.	Mhe. Ally R. Kalungwana	__	Mjumbe
7.	Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah	__	Mjumbe
8.	Mhe. Hadija Kombo Kibati	__	Mjumbe
9.	Mhe. Wenceslaus Kalogeries	__	Mjumbe
10.	Mhe. Warda O.Bazia	__	Mjumbe
11.	Mhe. Amina H.Zihuye	__	Mjumbe
12.	Mhe. Suzana P.Mtikwa	__	Mjumbe
13.	Mhe. Mizambwa R.Lugonzo	__	Mjumbe
14.	Mhe. Daudi Salum Mnadi	__	Mjumbe
15.	Mhe. Msasa Hamisi Mohamedi	__	Mjumbe
16.	Mhe. Kuruthum Mwisongo	__	Mjumbe
17.	Mhe. Gilbert B.Mtafani	__	Mjumbe
18.	Mhe. Zinduna Kombo Selemani	__	Mjumbe
19.	Mhe. Gabriel M.Temba	__	Mjumbe
20.	Mhe. Kifimbo S. Jumanne	__	Mjumbe
21.	Mhe. Peter Joel Dhahabu	__	Mjumbe
22.	Mhe. Ndulu Castory	__	Mjumbe
23.	Mhe. Dismas W. Makanjira	__	Mjumbe
24.	Mhe. Amini Tunda Abdallah	__	Mjumbe
25.	Mhe. Mudhihiri S. Shoo	__	Mjumbe
26.	Mhe. Hassan Maringo	__	Mjumbe
27.	Mhe. Zawadi M.Kidando	__	Mjumbe
28.	Mhe. Juma A. Tembo	__	Mjumbe
29.	Mhe.Scolastica W. Mkude	__	Mjumbe
30.	Mhe. Hamisi A. Kilongo	__	Mjumbe
31.	Mhe. Rashid Matessa	__	Mjumbe
32.	Mhe. Hilda B.John	__	Mjumbe
33.	Mhe. Samuel Msuya	__	Mjumbe
34.	Mhe. Latifa Said Ganzel	__	Mjumbe
35.	Mhe. Mabula R. Lusewa	__	Mjumbe
36.	Mhe. Milikiel M.Mahiku	__	Mjumbe
37.	Mhe. Madaraka Bidyanguze	__	Mjumbe
38.	Mhe. Dorothy J.Mwamsiku	__	Mjumbe

Wajumbe wasiohudhuria kwa taarifa.

1.	Mhe. Abdulazizi Mohamed (MB)	__	Mjumbe
2.	Mhe. Devotha Minja (MB)	__	Mjumbe
3.	Mhe. Dr. Christine Ishengoma (MB)	__	Mjumbe
4.	Mhe. Amiri Juma Nondo	__	Mjumbe
5.	Mhe. Regina R. Chonjo	__	Mkuu wa Wilaya ya Morogoro

Waalikwa waliohudhuria.

1.	Ndg. Christer B. Njovu	__	Kaimu Katibu Tawala Msaidizi, Huduma za Serikali za Mitaa Mkoa

Watendaji waliohudhuria

1.	Ndg. Neema Michael	__	Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa
2.	Ndg. Michael Waluse	__	Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa
3.	Ndg. Upendo Elias	__	Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa
4.	Ndg. Ruben Urasa	__	Kaimu Mchumi wa Manispaa
5.	Ndg. Winfred A. Kipako	__	AfisaTarafa wa Manispaa
6.	Ndg. Samwel Subi	__	Kaimu Afisa Mazingira na Usafishaji wa Manispaa
7.	Dr. Safia Kingwahi	__	Afisa Utamaduni wa Manispaa
8.	Ndg. Enedy Mwanakatwe	__	Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa
9.	Ndg. Jafari A. Makupula	__	Afisa Ununuzi na Ugavi wa Manispaa
10.	Ndg. Mohamed M.O. Chamzhim	__	Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa
11.	Eng. Mnene James	__	Meneja wa TARURA wa Manispaa
12.	Ndg. Waziri Kombo	__	Afisa Utumishi wa Manispaa
13.	Eng. Juma Gwisu	__	Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa
14.	Ndg. Gilbert Msemwa	__	Kaimu Afisa Mipangomiji na Mazingira wa Manispaa.
15.	Ndg. Feliciana Katemana	__	Mratibu wa TASAF Manispaa
16.	Ndg. Elineema Mtaita	__	Katibu TSC wa Manispaa
17.	Dr. Ikaji Z. Rashid	__	Mganga Mkuu wa Afya wa Manispaa
18.	Ndg. Ponceano Kilumbi	__	Mweka Hazina wa Manispaa
19.	Ndg. Abdul Buhety	__	Afisa Elimu Msingi wa Manispaa
20.	Ndg. Wilfred W.Mramba	__	Mwanasheria wa Manispaa
21.	Ndg. Rehema Adam	__	Mthibiti wa Ubora wa shule Wilaya
22.	Dr Janeth Barongo	__	Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa
23.	Ndg. Festus Herman	__	Afisa Biashara wa Manispaa

Sekretarieti

1. Ndg. Deogratias Butabile __ Katibu wa Mikutano
2. Ndg. Maria Leke __ Katibu wa Mikutano
3. Ndg. Theresia Mbena __ Katibu wa Mikutano
4. Ndg. Lilian Henerico __ Afisa Habari
5. Ndg. Sylvia Kahitwa __ Katibu wa Mikutano
6. Ndg. Daudi A. Kibwana __ Katibu wa Mikutano

HMM/BM//33/2019/2020 Kufungua Mkutano

Kabla ya kufungua Mkutano uliimbwa wimbo wa Taifa na Dua la kuiombea Halmashauri.

Mstahiki Meya aliwakaribisha Wajumbe na alifungua mkutano saa 4:51 asubuhi.

HMM/BM/34/2019/2020 Kuridhia agenda za Mkutano.

Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo:-

1. Kufungua Mkutano.
2. Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro.
3. Taarifa mbalimbali kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa
4. Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 31/10/2019 (Mkutano wa kawaida) na tarehe 27/12/2019 (maalum).
5. Yatokanayo na Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 31/10/2019 (kawaida) na tarehe 27/12/2019 (Maalum).
6. Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo za Halmashauri.

6.1 Kamati ya Fedha na Uongozi vikao vya tarehe 21/10/2019 (kawaida), tarehe 14/11/2019 (Kawaida), tarehe 26/11/2019 (Dharura), tarehe 12/12/2019 (kawaida), na tarehe 17/12/2019 (Dharura).

6.2 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kikao cha kawaida cha tarehe 15/10/2019 (Kawaida) na tarehe 12/12/2019 (Dharura).

6.3 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kikao cha kawaida cha tarehe 17/10/2019.

6.4 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI Kikao cha kawaida cha tarehe 16/10/2019.

6.5 Kamati ya Maadili ya Madiwani.

7. Kufunga Mkutano.

HMM/BM//35/ 2019/2020 Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa

1. Kuhusu Hoteli ya Step one - Msamvu

Hoja

Mjumbe mmoja alitaka kujua Hoteli ya Step One Msamvu inamilikiwa na nani?

Jibu

Ilielezwa kuwa Hoteli hiyo inamilikiwa na Kampuni ya Msamvu Properties LTD baada ya kulipa fidia kwa mmiliki wa awali kwa kuwa awamu ya pili ya mradi wa stendi ilijumuisha kujenga Hoteli ya Kisasa.

2. Kuhusu Ziara za Wataalamu kusikiliza kero za Wananchi kwenye Kata:-

Mjumbe mmoja alitaka kujua ziara za Wataalam kutembelea Kata kusikiliza kero za wananchi ni zoezi endelevu au la?

Jibu

Ilielezwa kuwa zoezi hilo ni edelevu kwa kuwa ni maagizo ya Serikali baada ya ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya ziara Mikoani na kusimamishwa na Wananchi kutoa kero zao hivyo aliagiza Viongozi waende ngazi za chini kuwasikiliza Wananchi na kuwatatulia kero zao.

HMM/BM//36/ 2019/2020 Taarifa mbalimbali kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa

Kuhusu zoezi la uandikishaji wa piga kura (BVR)

Mkurugenzi wa Manispaa alitoa taarifa kuwa zoezi la uandikishaji wapiga kura (BVR) katika Manispaa ya Morogoro litaanza tarehe 3/2/2020 na litaisha tarehe 9/2/2020. Zoezi hilo ni la siku saba hivyo Waheshimiwa Madiwani walijulishwa wawahamasishe Wananchi kujitokeza kujiandikisha katika zoezi hilo.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo.

HMM/BM/37/ 2019/2020 Kusoma na kuthibitisha mihtasari ya mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 31/10/2019 (Mkutano wa kawaida) na tarehe 27/12/2019 (Maalum)

Mihtasari haikuwa na masahihisho, hivyo ilithibitishwa kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi za mikutano.

HMM/BM/38/ 2019/2020 Yatokanayo na mikutano ya Baraza la Madiwani wa tarehe 31/10/2019 (Kawaida) na tarehe 27/12/2019 (maalum)

1. **Kuhusu hali ya barabara za Manispaa ya Morogoro**

   Azimio:
   Meneja wa TARURA wa Manispaa aliagizwa awe anawasilisha taarifa ya matengenezo ya barabara kwenye vikao vya Halmashauri

   Utekelezaji:
   TARURA Manispaa itakuwa inawasilisha taarifa zake kwenye vikao vya Halmashauri kama ilivyoelekezwa.

   Mjadala:
   Wajumbe walieleza kuwa mvua zilizonyesha zimeharibu barabara za Manispaa hivyo Wajumbe walitaka ufafanuzi wa jinsi ya kuzitengeneza

   Ufafanuzi:
   Ilifafanuliwa kuwa TARURA inaendelea kupokea taarifa ya barabara zilizoharibika ili kufanya tathimini na kuangalia bajeti kama zimetengewa fedha ili ziweze kutengenezwa na kama hazikutengewa fedha zitatengewa fedha, katika bajeti ya mwaka 2020/2021

2. **Kuhusu barabara ya kuelekea Zahanati ya Kilakala:**
   Azimio:
   Baraza lilielekeza kuwa Meneja wa TARURA aangalie uwezekano wa kutengeneza barabara inayoelekea Zahanati ya Kilakala.

Utekelezaji:
TARURA Manispaa ya Morogoro itaweka kwenye bajeti zake za matengenezo ya barabara ambazo zinaelekea kwenye maeneo ya huduma muhimu za kijamii na fedha zikipatikana barabara hizo zitajengwa.

Hoja:
Ilielezwa kuwa TARURA itafute fedha za dharura ili kutengeneza barabara ya Kilakala inayoelekea Zahanati.

Ufafanuzi:
Ilielezwa kuwa fedha za dharura zina utaratibu wake kuomba kuzitumia lakini TARURA imeitengea fedha za matengenezo barabara inayoelekea Zahanati ya Kilakala katika bajeti yake ya mwaka 2020/2021

3.0 Kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Daladala Mafiga

Azimio:
Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa na Meneja wa TARURA wa Manispaa wapitie upya gharama za ujenzi na mkataba ili kupunguza gharama za ujenzi na kazi hiyo iweze kukamilika tarehe 31/12/2019 badala ya mwezi Mei, 2020 kama ilivyoelekeza Serikali.

Utekelezaji:
Ushauri ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kupitia maeneo ambayo yataondolewa pasipo kuathiri utekelezaji wa mradi huo. Benki ya Dunia kupitia kikao kilichofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 10–13/12/2019, walitoa maelekezo kuwa mradi wa ULGSP utafungwa rasmi mwezi Juni, 2020. Mkandarasi anaendelea na utekelezaji ambapo matarajio ni kukamilisha mradi kabla ya muda wa mkataba.

Mjadala na Maamuzi:
Ilielezwa kuwa Kamati ya Fedha na Uongozi ilipita na kuona kuwa mapaa matatu ya majengo likiwemo la Utawala ni mafupi hivyo Baraza lilitaka kujua hatua zilizochukuliwa kurekebisha.

Ufafanuzi:
Ilielezwa kuwa mapaa ya majengo hayo yapo katika kiwango cha vipimo vya majengo ya Serikali urefu ni mita 3 lakini mapaa hayo urefu ni mita 3.2. Aidha sababu nyingine eneo husika lina upepo mkali.

Kuhusu vyoo kuwa mbali na Stendi:
Wajumbe walieleza kuwa vyoo vipo mbali na stendi hivyo Baraza lilitaka kujua kigezo gani kilichotumika?

Ufafanuzi:
Ilielezwa kuwa Halmashauri ilimtafuta Mhandisi Mshauri na alifanya "design" hivyo miundombinu hiyo ipo katika kiwango.

Kuhusu gharama za mradi kuwa kubwa kwenye baadhi ya maeneo katika ujenzi wa Stendi ya Daladala Mafiga:
Ilielezwa kuwa Kamati ya Fedha na Uongozi baada ya kupitia gharama za ujenzi ilibaini baadhi ya maeneo yalikuwa na gharama kubwa na kuelekeza kuwa fedha zipunguzwe ili fedha zitakazopatikana zitumike kufanya kazi nyingine .

Maamuzi ya Baraza la Madiwani:
Baraza liliamua kuwa vifaa/kazi zilizopangwa kwenye mkataba zisipunguzwe ila ziendelee kutekelezwa na Menejimenti iendelee kupunguza gharama ili kupata fedha ambazo zitatumika kufanya kazi nyingine. Kamati ya Fedha na Uongozi iliagizwa ifanyie kazi maelekezo hayo

4.0 Kuhusu mtambo wa kuchakata taka ili kutoa gesi katika soko la Mawenzi.

Azimio
Baraza liliagiza kuwa Menejimenti iwasiliane na Prof. Felista Mombo wa SUA aliyetengeneza mtambo wa kuzalisha gesi ili kujua gharama za kuukarabati/kuutengeneza na kuwasilisha taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi.

Utekelezaji
Mawasiliano na Prof. Felista Mombo yalifanyika, fundi aliyetengeneza anaitwa Urio anaishi Chalinze, amepanga kuja tarehe 30/01/2020 kwa ajili ya kukagua Mtambo wa gesi na kutoa gharama za matengenezo.

5.0 Kuhusu mashne za POS za kukusanyia Mapato ya ada za taka:

Azimio
Baraza liliagiza kuwa ifikapo tarehe 15 Januari, 2020, madeni yote ya mapato ya taka ngumu yawe yamepelekwa Benki.

Utekelezaji

Watendaji wa Kata wanaendelea kupeleka fedha Benki japokuwa kuna baadhi ya Kata hazijapeleka

Mjadala na Maamuzi

Kuhusu Watendaji wa Kata wanaodaiwa mapato ya taka ngumu na kupelekwa polisi .

Ilielezwa kuwa Kamati ya Fedha ya Uongozi haikukubaliana kuwa Watendaji wa Kata wapelekwe polisi. Baraza lilielekeza kuwa Menejimenti kabla ya kuwapeleka polisi Watendaji wa Kata wanaodaiwa ilipaswa iwafungulie mashtaka kwenye mamlaka zao za nidhamu. Aidha, waliokusanya mapato ni vikundi kazi lakini wahusika hawakupelekwa polisi badala yake Watendaji wa Kata waliokabidhiwa POS ndiyo waliopelekwa polisi. Aidha vikundi sita vilivyokopeshwa tripu za magari kwa ajili ya kubeba taka havijalipa lakini havijapelekwa polisi.

Baada ya mjadala huo Baraza liliamua yafuatayo:

Baraza lilielekeza kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ahakikishe kuwa linapotokea jambo lolote linalohusu watumishi wa Halmashauri alipeleke Kamati ya Fedha Uongozi na Baraza la Madiwani kushughulikiwa.

Agizo

Vikundi sita vya Usafi wa Mazingira vilivyokopeshwa tripu za kubeba taka Menejimenti iendelee kuvifuatilia ili walipe.

6.0 Azimio

Kila Diwani wa Kata aitishe kikao cha Baraza la Maendeleo la Kata ili wajadiliane kulipa madeni ya taka ngumu.

Utekelezaji

Kata zinazodaiwa zilifanya vikao na kujadili namna ya kulipa madeni ya taka ngumu. Kata zilizokamilisha kulipa madeni ni pamoja na Mji Mkuu, Mazimbu, Chamwino,Tungi na Sultani Area.

7.0 Kuhusu Paka na Mbwa wanaozurura hovyo:-

Azimio

Mkuu wa Wilaya aliagiza Mbwa na Paka wanozurura hovyo Mitaani wadhibitiwe.

Utekelezaji

Jumla ya Mbwa 89 wamekamatwa na mtego maalum na kazi bado inaendelea.

8.0 Kuhusu wananchi wanaolima mbogamboga na Mahindi kwenye maeneo ya mjini:-

Azimio

Mkuu wa Wilaya aliagiza kuwa wananchi waliolima mbogamboga na mahindi kwenye maeneo ya mjini waachwe wavune ila wasiruhusiwe kulima tena isipokuwa kwa Kata za pembezoni. Aidha wakazi wasimamiwe wasafishe maeneo ya makazi yao hadi kwenye mitaro ya barabara.

Utekelezaji

Wenyeviti na Watendaji wa Mitaa yote 294, Watendaji wa Kata zote 29 wameshirikishwa katika kusimamia utekelezaji wa azimio hilo kupitia barua **Kumb. Na. A20/MMC-2 /Vol.11/5** ya tarehe 20/01/2020. Aidha barua hiyo ilinakilishwa kwa Waheshimiwa Madiwani wote katika Kata 29.

9.0 Kuhusu wanaokaidi kutekeleza Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira

Azimio

Ifikapo tarehe 05/01/2020 Menejimenti impelekee taarifa Mkuu wa Wilaya kuhusu notisi zilizotolewa kwa waliokaidi kutekeleza Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira na hatua zilizochukuliwa.

Utekelezaji

Taarifa itawasilishwa kwa Mkuu wa Wilaya mara baada ya kupokea taarifa kutoka kwenye Kata.

10.0 Kuhusu upangishaji wa maeneo ya wazi

Azimio

Baraza liliagiza kuwa Menejimenti ifanyie kazi pendekezo la kukusanya kodi/mapato kwenye maeneo ya wazi

Utekelezaji

Kamati imeundwa kwa ajili ya kutambua maeneo ya wazi na maeneo ya barabara (hifadhi ya barabara)

11.0 Kuhusu vibali vya ujenzi na uvamizi wa maeneo ya wazi

Azimio

Baraza liliagiza kuwa wanaokiuka masharti ya vibali vya ujenzi wachukuliwe hatua za kisheria na watozwe faini kwa mujibu wa Sheria ya Vibali vya Ujenzi. Aidha wanaojenga bila ya kuwa na vibali vya Ujenzi watozwe faini ya asilimia 2 ya ujenzi.

Utekelezaji

Watu wanaokiuka masharti ya Vibali vya Ujenzi wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Vibali vya Ujenzi. Menejimenti ilijipanga kuendesha zoezi la ukaguzi wa vibali vya ujenzi kwa wote wanaojenga bila kuwa na vibali vya Ujenzi. Zoezi hili litafanyika Kata kwa Kata kuanzia mwezi Januari,2020.

Mjadala na Maagizo

Ilielezwa kuwa changamoto ya ujenzi holela na watu kujenga bila ya kuwa na vibali vya ujenzi bado ipo. Aidha viwanja vya wazi vimevamiwa na kujengwa hivyo iliagizwa ufuatiliaji uendelee kufanyika.

Agizo

Baraza liliagiza kuwa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira ishughulikie changamoto ya Ujenzi holela mjini, watu wanaojenga bila kuwa na vibali vya ujenzi na waliovamia na kujenga kwenye viwanja vya matumizi ya wazi na kuwasilisha taarifa kwenye mkutano ujao.

12.0 Kuhusu kutoza kodi kwenye kumbi za Mikutano na sherehe Azimio

Baraza liliagiza kuwa Menejimenti ifanyie kazi mapendekezo ya kutoza mapato kwenye kumbi za mikutano na sherehe za watu binafsi.

Utekelezaji

Agizo limetekelezwa kama ifuatavyo:-

i) Kuzungukia kumbi kwa kushirikiana na BASATA kubainisha kumbi hizo kwa kusajili na kuchukua malipo ya vibali vya mwaka 2019/2020 zoezi limefanikiwa na makusanyo yamefanyika ya kulipia vibali kwa shughuli katika kumbi sambamba na kusajili kumbi mpya **11** na vibali – kumbi **18.**

ii) Wanaoendesha shughuli za sanaa, Harusi na shughuli zote zinazohusika ukumbini kulipia Tshs. 20,000.00 na wameitikia wanalipia.

iii) Sherehe binafsi za nyumbani zinazohusisha ngoma zinalipiwa Tshs. 50,000.00 kwa siku na kuzingatia muda uliopangwa kuanzia saa 4 asubuhi hadi saa 12 jioni.

iv) Tozo kwa faini kwa wanaokiuka pia limetekelezwa ili kuhimiza wazingatie masharti na maelekezo ya vibali vinavyoelekeza.

Mjadala na Maagizo

Baraza liliagiza kuwa tozo za sherehe za ukumbini zitozwe kwa asilimia ya kiasi anacholipa anaekodishiwa badala ya Tshs. 20,000.00. Menejimenti iliagizwa ifanyie kazi asilimia itakayotozwa na kuwasilisha taarifa kwenye mkutano ujao

13.0 Kuhusu ukarabati wa ukumbi wa mikutano wa Manispaa

Azimio

Baraza liliagiza kuwa Menejimenti ikarabati ukumbi wa Mikutano wa Manispaa ili uwe wa kisasa sanjari na kuweka viyoyozi

Utekelezaji

Halmashauri imetenga kiasi cha **Tshs. 80,000,000.00** kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya ukatabati wa ukumbi wa Mikutano wa Manispaa. Aidha, gharama za ukarabati (BOQ) zinaendelea kuandaliwa.

14.0 Kuhusu kutoa ushuru katika shule za watu binafsi na vyuo.

Azimio

Baraza liliagiza kuwa Menejimenti ifanyie kazi mapendekezo ya kutoza ushuru kwenye shule za watu binafsi na vyuo vilivyopo Manispaa ya Morogoro.

Utekelezaji

Wamiliki wa shule wameshaandikiwa barua kupitia kwa Afisa Elimu Sekondari na Afisa Elimu Msingi. Hivyo inasubiriwa Maafisa Elimu waandae kikao.

15.0 Kuhusu kutoza ushuru wa huduma wa Manispaa (Manicipal Service Levy) katika Mabenki

Azimio

Menejimenti iliagiza ifanyie kazi namna ya kukusanya ushuru wa huduma za Manispaa (Manicipal Service Levy) katika Mabenki

Utekelezaji

Mabenki yote yanalipa ushuru wa huduma.

16.0 Kuhusu mapato ya maegesho

Azimio

Baraza liliagiza kuwa Manispaa na TARURA wakae pamoja kubainisha maeneo yanayopaswa kukusanywa kwa kila upande.

Utekelezaji

Vikao vya Wataalam vilikaa na kutatua mwingiliano wa maeneo mawili ambao yatakusanywa na Halmashauri. Maeneo hayo ni:-

1. Goldland
2. Flomi

Aidha, maeneo mengine Wataalam wanaendelea kuainisha kama vile:-

1. Lupila ambalo ni eneo la Manispaa lakini wanakusanya TARURA
2. SIDO ambalo ni eneo la Manispaa lakini wanakusanya TARURA
3. Mawenzi ambalo ni eneo la wazi (BIO GAS) eneo la Manispaa lakini wanakusanya TARURA
4. Manzese eneo la wazi la Manispaa lakini wanakusanya TARURA

Mjadala na Maagizo

(i) Baraza liliagiza kuwa Menejimenti iharakishe kufanya kikao na TARURA ili kubainisha maeneo ambayo Halmashauri na TARURA wanapaswa kukusanya.

(ii) Mapato waliyokusanya TARURA kwenye maeneo waliyostahili kukusanya Halmashauri fedha hizo TARURA wazirudishe au zigawanywe Manispaa na TARURA

17.0 Kuhusu ujenzi wa Soko Kuu na ujenzi wa Mto Kikundi.

Hoja

Mjumbe mmoja alieleza kuwa Soko Kuu lilitakiwa likamilike tarehe 31/12/2019 lakini ujenzi bado unaendelea hivyo alitaka kujua hatua gani zilizochukuliwa za kuchelewesha kazi. Aidha, Mzabuni anayejenga Mto Kikundi muda wake umekwisha hivyo naye atachukuliwa hatua gani za kuchelewesha kazi.

Pia ilielezwa kuwa Kata zinazopitiwa na Mto Kikundi zinapatwa na adha ya udongo uliyorundikwa kwenye hifadhi ya mto na kwenye baraza za nyumba hivyo kuwa kero kwa Wanachi

Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa Mkandarasi wa Soko Kuu aliongezewa muda hadi tarehe 30/03/2020. Aidha Mkandarasi wa Ujenzi wa Mto Kikundi aliomba kuongezewa muda hadi mwezi Mei, 2020.

Aidha, changamoto kubwa iliyopo ni mvua nyingi zilizosababisha mto kujaa maji.

Baraza lilipokea taarifa hizo na kuelekeza ushirikishwaji uwepo kuhusu namna ya kulipokea na kuliendesha Soko Kuu.

HMM/BM/39/2019/2020 Taarifa za Kamati za kudumu na kamati nyinginezo za Halmashauri

1.0 Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uongozi vikao vya tarehe 21/10/2019 Kawaida), tarehe 14/11/2019 (Kawaida) tarehe 26/11/2019 (Dharura) tarehe 12/12/2019 (Kawaida) na tarehe 17/12/2019(Dharura).

Taarifa iliwasilishwa na ilipokelewa na Wajumbe.

Mjadala

Kuhusu Vituo vya Afya na Zahanati zilizotembelewa ili kubaini changamoto na kuzitatua.

Hoja

Ilielezwa kuwa Kata ya Mindu Zahanati ya Mgaza inatoa huduma chini ya mwembe hivyo Mjumbe mtoa hoja alipendekeza ipatiwe fedha za matengenezo

Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa Zahanati ya Mgaza haipo kwenye bajeti hivyo itatengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2020/2021.

Baada ya mjadala Wajumbe waliridhia taarifa

2.0 Taarifa ya Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kikao cha kawaida cha tarehe 15/10/2019 na tarehe 12/12/2019 (Dharura)

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

3.0 Taarifa ya Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kikao cha kawaida cha tarehe 17/10/2019

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

4.0 Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kikao cha kawaida cha tarehe 16/10/2019

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

5.0 Taarifa ya Kamati ya Maadili ya Madiwani

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

HMM/BM/40/ 2019/2020 Kufunga Mkutano	Mstahiki Meya aliwashukuru Wajumbe kwa kuchangia hoja mbalimbali na kusisitiza ushirikiano kwa maendeleo ya Halmashauri. Alifunga mkutano saa 6: 57 Mchana.

Muhtasari umethibitishwa:- Tarehe ……

…….. ……. …….

Mhe. Pascal M. Kihanga — **MSTAHIKI MEYA MWENYEKITI**

Ndg. Sheilla E. Lukuba — **MKURUGENZI WA MANISPAA KATIBU**

YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 30/01/2020

MUHT. NA.	AZIMIO	MTEKELEZAJI	UTEKELEZAJI
HMM/BM/38/ 2019/2020 Yatokanayo na mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 31/10/2019 (Kawaida) na tarehe 27/12/2019 (Maalum)	**1.0 Kuhusu Gharama za mradi kuwa kubwa kwenye baadhi ya maeneo katika stendi ya daladala Mafiga.** Baraza liliamua kuwa vifaa/kazi zilizopangwa kwenye mkataba zisipunguzwe ila ziendelee kutekelezwa na Menejimenti iendelee kupunguza gharama ili kupata fedha ambazo zitatumika kufanya kazi nyingine. Aidha Kamati ya Fedha na Uongozi iliagizwa ifanyie kazi maelekezo hayo.	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Azimio litazingatiwa kama ilivyoelekezwa na Baraza.
	2.0 Kuhusu vikundi kazi vya Usafi wa Mazingira vinavyodaiwa tripu za kuzoa taka ngumu Baraza liliagiza kuwa vikundi sita vya usafi wa mazingira vilivyokopeshwa tripu za kubeba taka ngumu Menejimenti iendelee kuvifuatilia ili vilipe.	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Hadi tarehe 20/03/2020 vikundi 3 vilikuwa bado vinadaiwa **Tsh. 1,260,000.00**. Kiumu Cleaners **Tsh. 450,000.00**, Msimamo **Tshs. 250,000.00** na Mwale Cleaners **Tshs. 60,000.00**.
	3.0 Kuhusu vibali vya ujenzi na uvamizi wa maeneo ya wazi Kamati ya Mipangomiji na	Mwenyekiti wa Kamati ya	Agizo limezingatiwa. Kamati ya Mipangomiji na Mazingira katika kikao chake cha tarehe 14/01/2020 iliunda Kamati Ndogo ya kushughulikia suala hilo na taarifa

	Mazingira ishughulikie changamoto ya ujenzi holela mjini, watu waliojenga bila kuwa na vibali vya ujenzi na waliovamia na kujenga kwenye viwanja vya matumizi ya wazi na kuwasilisha taarifa kwenye mkutano ujao.	Mipangomiji na Mazingira	itawasilishwa katika Kamati hiyo kisha Baraza la Madiwani.
	4.0 Kuhusu kutoza kodi kwenye kumbi za mikutano na sherehe Baraza ililiagiza kuwa tozo za sherehe za ukumbini zitozwe kwa asilimia ya kiasi anacholipa anayekodishiwa badala ya shilingi 20,000.00. Menejimenti ifanyie kazi asilimia itakayotozwa na kuwasilisha taarifa mkutano ujao.	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Agizo limezingatiwa Tozo kwa kuzingatia 10% kwa anayekodisha limeanza kutekelezwa. Wahusika wanaelimishwa kuhusu hili na wanalipa kwa kuzingatia agizo hilo.
	5.0 Kuhusu Mapato ya Maegesho (i) Menejimenti iharakishe kufanya kikao na TARURA ili kubainisha maeneo ambayo Halmashauri na TARURA wanapaswa kukusanya	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Timu ya Wataalam kati ya Manispaa ya Morogoro na TARURA ilikaa tarehe 24/04/2020 ili kujadiliana vituo vitano (5) vinavyopaswa kukusanywa na Manispaa. Vituo hivyo ni eneo la wazi Mawenzi (kituo cha Bio gas), Manzese eneo la wazi, Sido, Lupila, na Goldland/Step 1. Baada ya maeneo hayo kuainishwa na majadiliano kufanyika TARURA ilikataa mapendekezo ya maeneo hayo kukusanywa na Manispaa, aidha Menejimenti imeitaka TARURA itoe majibu hayo kwa barua.

	(ii) Mapato waliyokusanya TARURA kwenye maeneo waliyostahili kukusanya Halmashauri fedha hizo TARURA wazirudishe au zigawanywe Manispaa na TARURA	Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi	Agizo limezingatiwa Menejimenti imemwandikia barua Meneja wa TARURA yenye Kumb. Na.F.10/MMC-16/77 ya tarehe 03/04/2020 kumtaka arejeshe fedha alizokusanya katika maeneo ya SIDO, Lupira, Goldland na eneo la wazi Mawenzi.